# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Pili – Tarehe 5 Aprili, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuweka mezani Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 10

### Hitaji la Hospitali ya Wilaya

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** Aliuliza:-

Wilaya ya Mlele haina Hospitali ya Wilaya.

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ya Mlele?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ni miongoni mwa vipaumbele vinavyowekwa na Halmashauri yenyewe. Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imepanga kuboresha Kituo cha Afya cha Inyonga ili kiweze kutoa huduma zenye hadhi ya Hospitali ya Wilaya katika kipindi cha mpito kabla ya kujenga Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hicho kwa sasa kina wodi nane zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 98 kwa siku, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la utawala lenye ofisi sita, stoo ya dawa, chumba cha maabara, chumba maalum cha upasuaji chenye vifaa vyote, mfumo wa maji safi na majitaka katika hospitali na matundu nane ya vyoo vya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazoendelea ni ujenzi wa jengo la upasuaji ambalo limefikia hatua ya lenta na jengo la kuhifadhia maiti *(mortuary)* ambalo limefikia hatua za umaliziaji. Ujenzi wa majengo hayo umeshagharimu shilingi milioni 418 na kazi inaendelea.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele tayari imeshatimiza masharti yote ya kujenga maabara, ya kujenga mfumo wa maji safi na taka pamoja na matundu nane ya vyoo; na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mlele hususan akina mama wa Tarafa ya Inyonga wanapata shida sana kwa ajili ya matibabu yao kwa sababu kile ni kuwa kituo cha afya lakini Halmashauri yao imefanya juhudi kubwa kwa matengenezo yote waliyoweka vigezo Serikali.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa kibali ili kile kituo cha afya kiweze kuwa Hospitali ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa yale maeneo ambayo yanajengwa majengo mengine wananchi hawajalipwa fidia zao, wanadai sasa muda mrefu hawajalipwa, ni lini Serikali itawalipa pesa zao ili wananchi wa Wilaya ya Mlele hususan Tarafa ya Inyonga waweze kupata pesa zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na mimi nakumbuka nilitembelea katika Mkoa wetu wa Katavi na miongoni mwa hospitali nilizokwenda kutembelea ni hiki Kituo cha Afya lakini kipindi kile kilikuwa kinakabiliwa na changamoto kubwa sana ya maji na nilitoa maelekezo pale na nimshukuru sana Mbunge wa Jimbo pale amefanya harakati imepatikana fedha hivi sasa mfumo wa maji umepatikana. Na bahati nzuri hospitali hii kwa watu wasiofahamu ni kwamba ni kweli miundombinu yote imekamilika, na siku ile nilitoa maelekezo kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Katavi kwamba sasa kwa sababu eneo lile ndiyo eneo la kimkakati na Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele yako pale Iyonga, nikasema kwa sababu vipaumbele vyote vinavyotakiwa na mahitaji yote yameshakamilika basi waanze mchakato kuhakikisha eneo lile sasa linakuwa rasmi, kituo kile kinakuwa rasmi kuwa Hospitali ya Wilaya ilimradi

waweze kukidhi vile viwango vya upataji bajeti inayolingana na hospitali ya Wilaya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Anna Lupembe naomba nikuhakikishie kwamba haya yalikuwa maelekezo yangu nilipokuwa kule *site* kutokana na mahitaji ya maeneo hayo yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala zima la wakazi waliokuwa pale; ni kweli, ukiangalia kwamba kuna nyumba nyingi sana zimejengwa katika maeneo yale na bahati mbaya sana kuna watu wanaotaka fidia pale na nilitoa maelekezo katika Halmashauri yetu sasa ipange mkakati jinsi gani wale watu wataweza kulipwa fidia. Kwa sababu eneo lile likishakuwa hospitali ya wilaya lazima tuwe na eneo la kutosha kwamba wananchi katika eneo lile na hospitali ile iwe na hadhi kwamba maeneo yale sio kuingiliwa na watu na nina imani kwamba katika vipaumbele vya bajeti ya Halmashauri mwaka huu itakuwa imetengwa hiyo. Lengo kubwa ni kuifanya hospitali ile sasa iwe rasmi kuwa Hospitali ya Wilaya.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Siha inafanana sana na Wilaya ambayo imetangulia kuulizwa hapa, na Mheshimiwa Waziri aliitembelea Hospitali yetu ya Wilaya ya Siha na ameona kwamba tuna wagonjwa wa nje tu, hatulazi lakini juhudi zinaendelea na hata wiki hii wananchi wamejitolea kuchimba msingi kwa ajili ya kuendeleza hospitali yetu na changamoto kubwa tuliyonayo ni watumishi, hospitali yetu haina watumishi na hata tukifikia mahali pa kulaza na kuweza kufanya *operation* na huduma nyingine hatutakuwa na watumishi na madaktari.

Je, anatuambia nini kwa sababu ndani ya mwaka huu tutaanza kulaza na kufanya *operation,* je, ni mkakati gani wa dharura utafanyika ili hospitali hiyo iweze kupata watumishi wa kutosha na kazi ianze?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifika pale Siha na nilivyofika pale licha ya hilo suala la watumishi lakini nilitoa maagizo. Serikali tumepeleka fedha pale kwa ajili ya kuhakikisha tunamaliza miundombinu katika ile *floor* ya juu, lakini nilitoa maagizo kwa sababu matumizi ya fedha zile, vikao vilivyokaa kwamba inaonkana fedha zile zilikuwa zinakwenda kutumika isivyo halali. Imani yangu ni kwamba katika eneo la Siha, utawala wa Siha utakuwa umefanya utaratibu mzuri jinsi gani tunaenda kupata *value for money* jengo lile linakamilika wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la watumishi sasa, Serikali inasema sio Siha peke yake, isipokuwa katika maeneo yote tuna changamoto sana ya watumishi na hasa katika suala zima la uhakiki tulivyopeleka hivi sasa kuna watu wengine walikimbia vituo.

Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba kwa sababu tuna mchakato hivi sasa wa suala zima la ajira nadhani Wizara ya Utumishi itakapokuwa tayari basi kibali kitatoka kuhakikisha kwamba tunapata waajiriwa mbalimbali katika sekta mbalimbali hasa ikiwa sekta ya afya na watakuja kule Siha kuwahudumia wananchi wa Siha.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala la Wilaya ya Mlele linafanana kabisa na suala la Wilaya ya Mvomero na kwa kuwa Wilaya ya Mvomero tayari tumeshajenga Hospitali ya Wilaya ambayo imekamilika kwa asilimia 80 na kwa kuwa kuna fedha ambazo tunazisubiri kutoka Serikalini ili tukamilishe na wananchi waanze kupata huduma; je, Serikali iko tayari kukamilisha ahadi yake ya kuleta zile fedha na hospitali ile iweze kufunguliwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam, Serikali

iko tayari na ndiyo maana katika kipindi cha sasa katika sekta ya afya tumekuwa tukipelekeza pesa nyingi sana katika eneo hilo, na ndiyo maana naomba nikuhakikishie sio suala zima la miundombinu hata katika suala zima la madawa tumefanya kazi kubwa sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Murad naomba tukitoka hapa tuwasiliane tuangalie jinsi gani katika bajeti yenu ya mwaka huu kipi kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo kuweza kumalizia, lakini jinsi gani tufanye tuweze kusukuma kwamba katika bajeti ya mwaka huu ambayo imetengwa tusukume ilimradi fedha zipatikane suala la ujenzi likamilike ilimradi wananchi wa Mvomero waweze kupata huduma ya afya kama inavyotarajiwa.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Na mimi naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Mlele linafanana sana na tatizo la Tabora Manispaa, Uyui pamoja na Kaliua, je, Serikali inasema nini kuhusu kukamilisha au kuandaa mpango wa kukamilisha hospitali ambazo hazipo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, Serikali kama tulivyosema kipaumbele chake ni kuhakikisha huduma ya afya inapatikana na ndiyo maana siwezi ku-*disclose information* zote, lakini kuna juhudi kubwa sana inafanyika lakini kiukweli ni kwamba kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwanza kipaumbele cha kwanza kinawekwa na Halmashauri, japokuwa mnajua kwamba katika suala zima la *cealing* ya bajeti wakati mwingine ile *cealing* ikishaondoka vipaumbele vingine vinakwama, lakini tutaangalia jinsi gani tutafanya, lengo letu kubwa ni kwamba wananchi katika kila maeneo waweze kupata huduma. Na ndiyo maana tunafanya harakati mbalimbali kufanya marekebisho makubwa katika sekta ya afya lakini imani yangu ni kwamba tutafika mahali pazuri tutasimama vizuri. Kwa hiyo wananchi, ndugu zangu wa Tabora ambao wengi ni watani wangu

naomba msiwe na hofu kwamba Serikali yenu iko nanyi kuhakikisha kwamba mambo yanakuwa mazuri.

Na. 11

**Ujenzi wa Chujio na Usambazaji wa Maji Mji Mdogo wa Mugumu**

**MHE. MARWA R. CHACHA** Aliuliza:-

Wilaya ya Serengeti ina Mbuga ya Wanyama ya Serengeti inayovutia watalii wengi duniani lakini inakabiliwa na uhaba wa maji.

Je, ni lini ujenzi wa chujio na usambazaji wa maji kutoka Bwawa la Manchira kwenda Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu na vijiji vya jirani utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa chujio na usambazaji wa maji Mji Mdogo wa Mugumu utakamilika na kuanza kutoa huduma ifikapo mwezi Juni, 2017. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.49 kupitia Mkandarasi *M/S Pet Cooperation* wa Kahama kupitia Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Mara. Utekelezaji wa mradi umekamilika kwa asilimia 62.5 ambapo mkandarasi ameshalipwa shilingi milioni 933.8.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza swali langu limejibiwa nusu, mimi nimeuliza ni lini ujenzi wa chujio na usambazaji wa maji utakamilika? Kwa hiyo, yeye amejibu upande mmoja wa ujenzi wa chujio, hajajibu upande wa usambazaji wa maji. Na ujenzi wa chujio

hili unasimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Maji pengine ndiyo maana Mheshimiwa Naibu Waziri hana picha halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza; la kwanza ni kuhusu usambazaji wa maji katika Mji wa Mugumu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa chujio hili. Nataka kumuuliza Naibu Waziri, bahati nzuri ulikuja mwaka jana pale Jimbo la Serengeti pale Mugumu na uliyaona yale maji, ninataka kujua kama kata zote za Mamlaka ya Mji mdogo wa Mugumu, kata saba Kata ya Morotonga, Kata ya Mugumu, Kata ya Stendi Kuu, Kata ya Getaisamo, Kata ya Kisangura kama zote zitapata maji, pamoja na vijiji vinavyozunguka lile bwawa, Kijiji cha Miseke, Kijiji cha Rwamchanga na Kijiji cha Bwitengi. Hilo ni swali la kwanza, ningependa kujua kwamba wakati wa usambazaji wa maji haya maeneo yote yatapata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha, swali la kwanza ameshaelewa, uliza la pili.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; huyu mkandarasi ambaye anajenga chujio hili *(PET)* anadai sasa hivi ana *certificate* ambayo iko Wizarani ya zaidi ya milioni 200 na kimsingi mradi ule unasuasua pengine kwa sababu hana fedha. Je, Wizara iko tayari kumlipa *certificate* anayodai ili aendelee na hii kazi mradi ukamilike haraka huo mwezi wa sita?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa hii awamu tulianza kujenga chujio ili kuongeza uzalishaji wa maji ifikie lita milioni tano kwa siku, ambazo zinatosha kwa wakazi kwa sasa kwa wale wa mjini, lakini Serikali kwa kutumia mkopo wa dola milioni 500 tumetenga milioni nane *US dollars* ambazo ni sawasawa na shilingi bilioni 19 kwa ajili ya kuboresha usambazaji katika maeneo ya vitongoji vya Mji wa Mugumu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na shaka, tatizo la kupata maji ya uhakika kwa Mji wa Mugumu na vitongoji vyake linashughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili kuhusu madai ya mkandarasi; madai hayo tutamlipa mara tu baada ya kupata hizo *certificates,* hakuna shaka ya fedha, fedha tunazo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge anasema zipo Wizarani kwa hiyo, wataalam watusaidie, kama zipo wakukabidhi Waziri.

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Cecilia Paresso ulikuwa umesimama.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kama ambavyo Wilaya ya Serengeti inazungukwa na mbuga ya wanyama, vivyo hivyo Wilaya ya Ngorongoro ina changamoto kubwa sana ya kijiografia kutoka tarafa moja kwenda tarafa nyingine ni kilometa nyingi ikiwemo kutoka Tarafa ya Ngorongoro kwenda Tarafa ya Loliondo ambapo kuna takribani kilometa mia na zaidi, na Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika umejionea mazingira ya Ngorongoro.

Je, Serikali iko tayari sasa, kulingana na ugumu wa jiografia ya Ngorongoro, kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi hao inapatikana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifika Ngorongoro takribani wiki tatu na nusu zilizopita, na ni kweli jiografia ukitoka hapa Karatu wakati unatoka getini pale mpaka unafika kule Loliondo ni mbali sana na sio hivyo tu, nilifanya jiografia pana sana nikazunguka lile Jimbo la Ngorongoro nikapita mpaka katika Ziwa Natron pale, kweli changamoto ya maji ni kubwa na kama nilivyokuwa kule *site* niliahidi kwa wananchi kwamba tutafanya kila liwezekanalo kushirikiana na Halmashauri ile ya Ngorongoro kuangalia jinsi gani tutafanya kuhakikisha kwamba tunapata ujenzi wa maji kule kama ni *borehole* au vyovyote.

Kwa mfano ile Shule ya Sekondari ya Ziwa Natron pale, watoto wako pale lakini na maji yapo pale ila isipokuwa jinsi gani kuyasambaza kufika shuleni. Kwa hiyo, vyote nimeenda kule nimeweza kufanya *needs assessment* ya eneo lile na naomba nikuhakikishie kwamba kama Serikali na matakwa yetu ya Kiserikali tutafanya kila liwezekanalo kuwasaidia wananchi wa Ngorongoro.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri, alipotembelea Wilaya ya Korogwe aliweza kuona hali halisi ya tatizo la maji lililopo katika mji wetu wa Korogwe. Hata hivyo aliahidi kutuletea shilingi bilioni mbili ili angalau tatizo la maji lile liweze kuondoka pale, swali; kwa kuwa wameshatuletea milioni 500 kwa ajili ya kutoa maji kutoka kwenye Mto Ruvu, je, sasa Serikali zile fedha wameshaziingiza kwenye bajeti ili kusudi ziweze kutusaidia katika kutengeneza miundombinu ile ambayo ni mibovu maana yake tutakapokuwa tumejenga matenki au tumejenga ule mkondo wa maji bila ya kuwa na matenki ya maji makubwa bado tatizo la maji litakuwa lipo pale Korogwe. Je hizi fedha shilingi bilioni mbili alizosema zimetengwa katika bajeti hii? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:**Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulitenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuboresha maji katika Mji wa Korogwe na tulitoa maelekezo kwamba usanifu ukikamilika tunatangaza *tender* kwa hiyo ikishatangazwa *tender* na wakianza kufanya kazi tutakuwa tunalipa kwa *certificate* jinsi zinavyokuja. Kwa hiyo, naomba nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule utatekelezwa na fedha zipo kwenye bajeti. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali swali la nyongeza.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Suala hili la maji kwenye Kijiji changu na Kata ya Zinginari kuna mradi wa maji ambao unagharimu shilingi milioni 400 umefanywa, muda umeisha lakini mpaka leo maji hayatoki, kimekuwa ni kilio kikubwa sana.

Je, Waziri anafahamu kwamba kuna hii shida na kama afahamu atakuwa tayari kwenda na mimi kwenye Jimbo langu ili ashuhudie namna ambavyo shilingi milioni 400 hizi zimeliwa na maji hakuna? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:**Mheshimiwa Suleiman Jaffo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kesi mbalimbali na kuna baadhi ya maeneo mengine kwamba miradi imetekelezwa lakini wakati mwingine maji hayajapatikana na hii ina maana kwamba inatofautiana kutokana na mazingira. Mengine ni suala zima wakati mwingine zimechimbwa *borehole* ambapo zile *borehole* wakati mwingine zinakosa maji, lakini sehemu zingine ni suala zima la usimamizi na uzembe katika usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kulijua kwa kuona jambo hilo kwasababu ni maeneo ya Kilombero peke yake ambayo nilikuwa bado sijafika katika Mkoa wa Morogoro na ni imani yangu hata katika Bunge hili la Bajeti nitafika kule Kilombero. Basi naomba nikifika kule tuweze kuangalia jinsi gani tatizo lililoko pale halafu tulipatie tiba halisia kutokana na jinsi tutakavyoliona lengo kubwa ni kwamba Wananchi wa eneo lako waweze kupata huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.12

**Kukamilika kwa Miradi ya Maji Wilaya ya Sengerema**

**MHE. KEMIREMBE J. LWOTA** Aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha miradi ya maji inayojengwa Wilayani Sengerema katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa inakamilika haraka na kuwanufaisha wananchi wa Buchosa hasa mradi wa maji wa Lumea - Kalebezo na Nyegonge?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Sika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mitatu inayohudumia vijiji nane katika Halmashauri ya Buchosa inaendelea kujengwa ambayo ni mradi wa maji Lumea - Kerebezo - Nyegonge, mradi wa maji Nyakalilo - Bukokwa na mradi wa maji Luchili - Nyakasungwa hadi Igwanzozuna.

Ujenzi wa mradi wa maji Lumea - Kalebezo - Nyegonge ulianza kutekelezwa mwezi Machi 2013 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.69 kwa sasa mradi huo upo katika hatua za mwisho za majaribio ya mitambo pamoja na miundombinu na utaanza kutoa huduma ifikapo Juni, 2017. Mradi utakapokamilika utanufaisha wakazi 16,000 wa vijiji vya Kalebezo na Nyegonge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kemirembe Lwota swali la nyongeza.

**MHE. KEMIREMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ila nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika wote tunafahamu tatizo la maji na tunajua kabisa maji ni uhai na hakuna Mbunge hata mmoja humu ndani ambaye tutamsimamisha ambaye Jimbo lake halina tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika ifike mahali kama Serikali tuwe na vipaumbele vichache ambavyo tutaweza kuvitekeleza kiuhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, katika mradi huo wa Nyamazugo - Buchosa mradi huo wa maji unapita katika vijiji vya Isenyi, Nyamabanda na Nyanzenda ambapo ndiyo chanzo cha maji kinaanza na unaenda kutekelezwa kwenye vijiji vingine zaidi, swali langu, ni lini Serikali itafikisha maji katika vijiji hivi vichache ambavyo maji yanapita na kwenda kutekelezwa kwenye vijiji vingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Wilaya ya Sumve kwenye vijiji vya Kadashi na Isunga kumekuwepo na mradi wa maji ambao umekaa unasuasua kwa miaka mingi. Je, ni lini Serikali itamaliza mradi huu wa Wilaya ya Sumve? Ahsante

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mbunge ni kwamba kuna chanzo cha maji lakini kuna vijiji jirani ambapo maji yanatoka kwamba kwa mujibu wa *design* vijiji vile vitakosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tufanye rejea ya Mheshimiwa Waziri wa maji kwamba na Waziri wa Nishati na Madini kwamba kwa mkakati wa Serikali ya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo vyanzo vinapatikana basi vitapewa kipaumbele jinsi gani kuweka *design* kama mwanzo vilisahaulika kuweka utaratibu wa kuweka *design* nzuri ya kuhakikisha maeneo yale ambayo vyanzo vinapatikana yaweze kupata maji.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishie kwamba Serikali hii itafanya kila liwezekanalo wananchi wa eneo lako lile lazima wapate maji kutokana kwamba lazima Serikali iweze kuwahudumia wananchi wale, lakini siyo hivyo tu, na wao watasaidia kuweza kulinda vizuri chanzo cha maji katika eneo lile. Lakini katika eneo la Sumve ni kwamba kuna mradi wa maji lakini mradi huu unaonekana kwamba haujakamilika, ni *commitment* ya Serikali na naomba tufahamu, siyo mradi huo peke yake karibu kuna miradi mingi sana ilianza kutekelezwa lakini mingi ilisimama huku nyuma naona *flow* ya fedha ilikuwa siyo nzuri, lakini hivi sasa kwa Seriakli ilivyojipanga ni kwamba mradi sasa hivi mkandarasi akikamilisha kazi, aki-*submit certificate* maana yake *certificate* inalipwa na mkandarasi anaendelea kufanya kazi.

Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba Serikali itajitahidi kwa kadri iwezekanavyo miradi yote ambayo ilikuwa ime-*stuck* sasa wakandarasi waweze kutimiza wajibu wao, wakamilishe ile miradi, wa-*raise certificate* zitalipwa ilimradi lengo la miradi iweze kukamilika na miradi hiyo iweze kuwapata wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela swali la nyongeza.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Waziri nilitaka kufahamu wakazi wa Mkoa wa Katavi wamekuwa wakisubiri sana mradi ambao unaendelea kujengwa mradi wa maji wa Ikolongo B, wakazi wa Kata ya Ilembo, Misunkumilo, Kakese pamoja na maeneo mengine mradi huu umepita nyuma ya hizo Kata, lakini wakazi hawa wanakosa maji lakini pia wanatumia maji ambayo ni mchafu ya kutoka kwenye mabwawa pamoja na mito.

Sasa naomba unieleze kwamba ni lini mradi huu utakamilika kwa sababu Serikali tayari ilishatenga pesa lakini mradi bado unasuasua? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna baadhi ya sehemu zingine kwamba miradi inasuasua na mnakumbuka kwamba hata Mheshimiwa Rais alivyofika Mkoa wa Lindi aliweza kutoa maelekezo mahususi kwa mkandarasi anaejenga mradi wa maji pale katika Mji wa Lindi na hii ina maana kwamba maana yake ni maeneo mbalimbali kulikuwa na tatizo kubwa hasa baadhi ya wakandarasi wanaoshindwa kutimiza vizuri wajibu wao, wengine wameomba kazi lakini baadae wakienda kule *site* wanashindwa kutimiza wajibu wao, lakini naomba nikuhakikishie kwamba Serikali hivi sasa inafanya *vetting* kwa Wakandarasi wote ambao wanashindwa kutimiza wajibu wao, lengo kubwa ni kwamba atakaposhindwa bora atolewe aletwe mkandarasi mwingine aweze kutimiza wajibu wale na Mkandarasi huyu tutaenda ku-*assess* kazi yake inaendaje.

Lakini hata hivyo ulizungumza ajenda suala zima la kwamba Wananchi wengine ambao wa maeneo yale wanakosa maji, tutafanya mahitaji halisi kuangalia kwa sababu siwezi kuzungumza hapa moja kwa moja kule *site* sijaangalia lakini najua suala hilo linamhusu hata ndugu yangu Richard Mbogo, Mbunge wa Nsimbo pale nilivyofika nae ana hoja hiyo hiyo inayolingana ni kwamba tutaangalia kwa kina tutafanyaje lengo kubwa ni kwamba wananchi wote wa Tanzania kama lengo la Serikali hii kuwatua wakina mama ndoo ya maji liweze kufikia; haliwezi kufikia lazima tupambane wote kwa pamoja, aliyekuwa mzembe tumtoe katika daraja hilo la uzembe awe katika suala zima la sawa sawa wananchi wapate huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maige swali la nyongeza.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Serikali ilikamilisha mradi wa maji wa Ziwa Victoria mwaka 2008 na kwa bahati mbaya kuna baadhi

ya vijiji ambavyo bomba limepita kwenye vijiji hivyo vikawa vimesahaulika na toka mwaka 2014/2015 vijiji kama Kabondo, Mwakuzuka, Matinje, Buluma, Mwaningi ambavyo bomba limepita wala si kilometa 12 bomba limepita kabisa kwenye vijiji hivyo viliwekwa kwenye mpango kwamba vingepatiwa maji lakini hadi sasa vijiji hivyo havijapata maji kwa sababu fedha hazijatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusikia uhakikisho kutoka kwa Waziri kwamba ni lini sasa vijiji hivi vitapata maji kama ilivyokuwa imeahidiwa toka miaka yote niliyoisema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ajenda inayozungumzia ni suala zima la mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambayo hivi sasa hata ukiangalia mradi huu hata watu wa Tabora hujo watakuja kusimama mpaka Sikonge, lakini kuna mpango mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba maji haya yanafika mpaka Tabora mpaka Sikonge, lakini kuna changamoto ya baadhi ya vijiji vingine vilivyopitiwa lakini maji havikupata na Mheshimiwa Waziri wa maji alikuwa akizungumza mara kadhaa hapa Bungeni kwamba lengo kubwa la Serikali ni kuangalia kwa sababu maji yanakwenda kwa utaratibu maalum, lazima yafike katika tanki halafu yaweze kurudi kwahiyo yote inatakiwa ku-*design* ili iweze kufanyika lakini Waziri hapa alizungumza mara kadhaa kwamba kuangalia jinsi gani watu wote waliopitiwa katika bomba la Ziwa Victoria wataweza kupata maji.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwa *commitment* ya Serikali abayo inaiweka kwa wananchi wa Tanzania na hasa wale wanaopitiwa katika bomba kubwa la Ziwa Victoria ni kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha ni jinsi gani maji sasa maji yaweze kuwafikia Wananchi wako na wewe mwisho wa siku ni kwamba tuweze kukuona hapa Bungeni kwa heshima kubwa ya Wasukuma wa kule.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana, naomba nimuulize bwana Waziri; katika Wilaya ya Kwimba kuna vijiji kumi ambavyo vilipangiwa kupelekewa maji katika mradi wa vijiji kumi, zaidi ya miaka kumi leo, naomba leo nijue katika hivi vijiji vya Kadashi, Isunga, Shirima na Mhande mkandarasi hayupo *site* mpaka leo na kwa sababu nilishafanya mawasiliano na Mheshimiwa Waziri wa Maji mwenyewe kwa muda mwingi, nataka leo anipe majibi kazi hii ya miradi hii ya maji katika Wilaya ya Sumve na Kwimba lini itakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Aahh, nilifikiri Waziri wa Maji anataka kusimama. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge haongopi na mimi naomba nikiri kwamba nimefika Jimboni kwake kule na miongoni mwa jambo katika taarifa ambayo niliyosomewa ni changamoto ya maji na hali kadhalika suala zima la vijiji kumi katika suala zima la mpango wa *World Bank* na ni kwa sababu nimesema hapa nyuma kwamba miradi hii ya maji maeneo mengi sana ilisimama na ilisimama kwa sababu hapa nyuma suala zima la kifedha lilikuwa siyo zuri zaidi, lakini sasa hivi Serikali katika Mfuko wa Maji tumejipanga vizuri kuhakikisha miradi hii inatekelezeka.

Lakini jambo lingine utakuta kuna changamoto ya mkandarasi, kwa hiyo kwa sababu taarifa zimeshakuja Serikalini na Waziri wa Maji taarifa hii anayo sasa kwa kina basi nadhani mpango mzuri utafanywa naamini jambo hili litafanyika vizuri na miradi hii itakamilika na wananchi wa Jimbo lako watapata maji kwa sababu *commitment* ya Serikali hii kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Kusitisha Usafirishaji wa Gesi Kutoka Mtwara - Kinyerezi**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** Aliuliza:-

Gesi inayochakatwa Mtwara huweza kuzalisha viwanda vidogo vidogo ikiwemo mbolea na kwa miaka mingi wananchi wa Mtwara wamekosa fursa ya ajira ukilinganisha na maeneo mengine ya Tanzania kama vile Arusha, Mwanza, Kilimanjaro na kadhalika.

Je, ni lini Serikali itasitisha usafirishaji wa gesi kutoka Mtwara kwenda Kinyerezi ili wana Mtwara waweze kunufaika na ajira zinazotokana na uchakataji wa gesi hiyo asilia kufanyika Mtwara na Seriakli kujenga viwanda vitokanavyo na gesi Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera mpya ya Nishati ya mwaka 2015 na Sera ya Gesi Asilia ya mwaka 2013 zinalenga kutoa fursa ya rasilimali ya gesi asilia kuwanufaisha Watanzania wote wakiwemo wananchi inapopatikana rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika hadi sasa kuna miradi miwili inayosafirisha gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam. Miradi hiyo ni mradi wa kusafirisha gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam uliokamilika mwaka 2015 na mradi wa *Songas* uliokamilika mwaka 2004. Gesi inayochakatwa inasafirishwa kwa bomba kwa maeneo mbalimbali nchini yakiwemo kwa ajili ya maeneo ya Mtwara, Lindi, Mkuranga na Dar es Salaam. Visima viwili vya gesi asilia

katika eneo la Mnazi bay vimetengwa rasmi kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na gesi asilia kutoka Lindi na Mtwara kutumika kuzalisha umeme kwa asilimia 50 pia gesi hiyo inatumika katika kusambaza gesi majumbani na viwandani katika maeneo mbalimbali. Kwa sasa Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa *(TPDC)* inatekeleza mradi wa kuunganisha gesi hiyo katika Kiwanda cha Dangote kilichipo Mtwara ambacho kinahitaji futi za ujazo milioni 45. Pia shirika hilo liko kwenye majadiliano na kiwanda cha *URANEX* kinachotarajia kujengwa Mkoani Lindi ili kuweza kuunganisha gesi asilia hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha Nachuma swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 wananchi wa Mtwara waliweza kuandamana kwa kiasi kikubwa sana Mtwara na Lindi wakidai namna gani kwamba rasilimali hii gesi inaweza kuwanufaisha na tunashukuru hivi sasa manufaa hayo yanaanza kuonekana. Nilikuwa naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ule mpango wa kuwapa wawekezaji ambao wana nia ya kuwekeza Mtwara gesi waweze kutengeneza ama wajenge viwanda vya mbolea umefikia wapi mpaka hivi sasa?

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kujua, kulikuwa na mkakati na mwaka jana tulielezwa ndani ya Bunge hili kwamba kuna usambazaji wa gesi asilia kwenda majumbani kwa mana kwamba mikoa ya Dar es Salaam na maeneo mengine. Nilikuwa naomba kujua mkakati huu kwa Mkoa wa Mtwara na Lindi upoje kwa sababu tulipewa tu taarifa kwamba upembuzi yakinifu umeshaanza nataka kujua mimi kama Mbunge sina taarifa nao. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Kalemani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Maftaha kwa kweli kati ya Wabunge ambao wanahangaikia sana maslahi ya wananchi wake ni pamoja na Mheshimiwa Maftaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusuaiana na maswali yake ya msingi kabisa, kwanza kabisa ujenzi wa kiwanda cha mbolea Mtwara; nataka tu nimwambie Mheshimiwa Maftaha pamoja na wananchi wa Mtwara na Lindi kwamba hatu ailiyofikiwa sasa hivi; kwanza kuna Kampuni ya *HELM* kutoka Ujerumini imeshapata eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha mbolea na makadirio ya kukamilisha ujenzi huo ni mwaka 2020 lakini hata hivyo nimwambie tu hatua ambazo zinafanywa na Serikali.

La kwanza kabisa; Serikali kupitia *TPDC* wanafanya majadiliano sasa ya kuelewana sasa bei ya kununua gesi kati ya *TPDC* pamoja na Kampuni ya *HELM* itakayojenga kiwanda hicho na kwa sasa wameshaonesha kutenga jumla ya dola za Kimarekani milioni 200 kwa kampuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini taratibu za kuuziana gesi wakishamaliza kujenga ujenzi huo 2020 wataweza kupewa gesi na mahitaji ya kiwanda hicho cha mbolea inafikia milioni 80 futi za ujazo mpaka 104; kwa hiyo matarajio yapo na wananchi wa Mtwara watanufaika na kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la pili; ni kweli kabisa tulitarajia sana tuanze usambazaji wa gesi majumbani katika mji wa Mtwara na Lindi na Dar es Salaam pia, lakini tumefikia hatua nzuri. Upembuzi yakinifu umekamilika, matarajio yameshapatikana na kwa sasa Mtwara na Lindi wanahitaji milioni tano za gesi hadi kumi futi za ujazo ambazo zinagharimu shilingi bilioni mbili, Kwa hiyo kuanzia Julai mwaka huu, Wananchi wa Mtwara, Lindi na

Dar es Salaam wataanza sasa kupata gesi ya majumbani. Na Mheshimiwa Maftaha wale wananchi wako wale wa Mbawala chini pamoja na Mtajitambua wataanza kupata gesi asilia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Ziwa Tanganyika ni eneo ambalo kumefanyika utafiti wa gesi na mafuta hasa kwenye Tarafa ya Karema. Eneo hilo kuna uhakika wa kupatikana mafuta na gesi, je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Katavi na ukanda mzima wa Ziwa Tanganyika juu ya utafiti ambao umefanywa mpaka sasa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, majibu ya swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa utafiti umeshaanza kufanyika katika Ziwa Tanganyika ili kugundua gesi iliyopo na makampuni yaliyopita kufanya ni makampuni mawili ya Chuo Kikuu cha Ujerumani pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wanajiolojia wa Tanzania pamoja na *TPDC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika sasa ni kuanza kufanya *appraisal* ili kujiridhisha na gesi iliyopatikana. Zipo dalili za kugundua lakini kinachofanyika sasa ni*appraisal* na shughuli ya kukamilisha *appraisal* itafanyika mwezi Agosti mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo baada ya Agosti mwaka huu Mheshimiwa Kakoso wananchi wanaozunguka Ziwa Tanganyika wataanza kupata gesi asilia katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo; zipo hisia kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwamba Wizara ya Nishati na Madini haina nia ya dhati na kiwanda cha mbolea cha Msanga Mkuu cha *HELM* ambacho amekielezea uwekezaji wake. Kwa sababu majadiliano yamechukua muda mrefu na ujenzi ambao ameusema utakamilika mwaka 2020 kuanza kwake ujenzi itategemea makubaliano ya bei ya kuuziana gesi.

Je, anatoa kauli gani juu ya hisia za wananchi wa Mtwara kwamba kiwanda hcho hakitazamwi vizuri ndani ya Wizara yake hasa ukizingatia hata kwenye jibu lake la msingi hakukitaja kiwanda hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Dkt Kalemani majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Ghasia katika jibu langu la nyongeza nimeeleza mikakati ya Serikali ya kujenga kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimeeleza hatua ya majadiliano ya gesi kwa sasa nikupe taarifa Mheshimiwa Hawa Ghasia na mimi nakushukuru sana unavyohangaikia maendeleo ya wananchi wa Mtwara Vijijini, Kampuni ya Helmo kutoka Ujerumani inapendekeza kwa sasa hivi ichukue gesi kwa dola 2.6 wakati ukifanya hivyo Mheshimiwa Hawa na wewe unajua makadirio ya gharama ya chini kabisa katika *standard price* ulimwenguni kote na hapa kwetu ni dola 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Ghasia nikuhakikishie tu jitihada za makusudi zinafanyika kuhakikisha kwamba wananchi wa Mtwara wanapata gesi, lakini matumizi ya mbolea pia. Kwa hiyo, hatua tunayochukua

nataka nikuhakikishie kwamba kuja kufikia mwezi Julai majadiliano kati ya Kampuni ya *HELM* kwa kiwanda cha mbolea pamoja na Serikali yatakuwa yamekamilika na kiwanda cha mbolea kitaanza sasa kutekeza katika ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 waliosema ni makadirio yao ya kampuni kuwa wamesha-*set* taratibu zote na ujenzi wa kiwanda hicho kukamilika. lLakini jitihada za Serikali ziko pale pale. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Wilaya ya Liwale iko katika Mkoa wa Lindi na ndiyo Wilaya pekee ambayo bado mpaka leo hii inatumia umeme wa mafuta na mashine zile tumezitoa Rufiji, mashine zile zimechoka. Nini kauli ya Serikali kuipatia umeme wa gesi Wilaya ya Liwale ili tuweze kuwa na umeme wa uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa katika umeme tunaotumia hapa nchini 50% ya umeme tunaotumia unatokana na rasilimali ya gesi. Kwa hiyo, hata huko Liwale tunachofanya sasa hivi tunajenga miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Mtwara kuja Lindi utakaokwenda katika Wilaya za Liwale, Tandahimba, Nanyumbu pamoja na Masasi umbali wa kilometa 80 ili kupunguza umbali wa kilometa 206 zilizopo sasa. Lengo ni kuunganisha umeme wa gesi katika maeneo yote ya Mtwara na Lindi na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Liwale tunakuhakikishia kwamba kwa sasa hivi hata wananchi wa Liwale sasa wataanza kutumia umeme wa gesi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Tatizo la Umeme Mikoa ya Lindi na Mtwara**

**MHE. KAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA** Aliuliza:-

Serikali iliwaahidi wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi umeme wa uhakika na wa kutosha baada ya kugundulika kwa gesi na baada ya neema ya muda mfupi hivi sasa kuna tatizo kubwa la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Mikoa hiyo ikiwemo na Wilaya ya Newala.

Je, tatizo ni nini na Serikali inachukua hatua gani kumaliza kabisa tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kukatika kwa umeme mara kwa mara katika maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara inatokana na ubovu wa jenereta moja kati ya tisa katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia kilichoko Mtwara chenye jumla ya MW 18 ambayo imepungua hadi MW 16. Tatizo lingine ni uchakavu na urefu wa njia inayosambaza umeme wa msongo wa kilovoti 33 kutoka Mtwara kuelekea Wilaya za Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi – Nanyumbu- Nachingwea hadi Ruangwa ambao ni umbali wa kilometa 206.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kuondoa tatizo hilo ni pamoja na kufanya ukarabati wa mtambo ulioharibika ili kurudisha uwezo wa kituo katika

kuzalisha hali yake ya kawaida MW 18. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango mwingine ni kuongeza mitambo mingine sita yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa jumla ya MW 12 kila moja itakayofikisha MW 30 ambao unatosheleza kwa mahitaji ya mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha hali ya upatikanaji endelevu wa umeme katika Mikoa hiyo, *TANESCO* inajenga njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilometa 80 kutoka Mtwara hadi Mnazi Mmoja, Lindi. Kazi hiyo inajumuisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme msongo wa kilovoti 132/33 na transfoma za MVA 20 kwa ajili ya kusambaza umeme wa njia tano. Mradi huu unakamilika mwishoni mwa mwezi Mei, mwaka huu na gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 16.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkuchika swali la nyongeza.

**MHE. KAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Napenda kuipongeza Serikali kwa kusambaza umeme *(REA II)* vijiji karibu Tarafa zote sita za Wilaya ya Newala. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanaonesha kwamba tatizo la umeme maeneo ya Mtwara Mjini, Lindi yataisha na tumeshuhudia juzi Rais ameweka jiwe la msingi, lakini upande mwingine Naibu Waziri anakubali kwamba Wilaya za Tandahimba, Newala, Masasi, Nanyumbu, Nachingwea na Ruangwa hali ya upatikanaji wa umeme si nzuri na kule tatizo si kwamba umeme haupo tatizo ni miundombinu. Nyaya zimekatika, ikinyesha mvua nguzo imeanguka, ni lini Serikali itachukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba kukatikakatika kwa umeme na kuanguka nguzo kuna malizwa mara moja ili Wilaya hizi nazo zifaidi umeme kama wanavyofaidi Wilaya zingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, pamekuwepo na matamshi mengi upande wa Serikali juu ya gharama halisi za mwananchi wa kawaida kuingiza umeme katika nyumba yake. Nini kauli ya leo ya Serikali kwamba kijiji fulani kinataka kuingiza umeme pale Newala, yule mwananchi wa kawaida anatakiwa alipe shilingi ngapi kwa sababu matamko ya huko nyuma hayafanani na gharama halisi ambazo zimekuwa zikilipwa? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mkuchika jinsi ambavyo anashughulikia maslahi ya umeme ya wananchi wa Newala Mjini, nampongeza sana. Lakini pamoja na hayo, Mheshimiwa Mkuchika niseme tu maana hapa tutakaa tutajadiliana zaidi kwa sababu najua unafuatilia mambo yao sana na sisi kama Serikali tusingekuwa tayari kukuangusha, kwa hiyo, tunakuomba sana uendelee kutupa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na maswali yake mawili ya nyongeza; la kwanza kabisa, ni lini Serikali sasa itachukua hatua za kutatua tatizo la kukatikakatika kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo katika maeneo hasaa ya Mtwara na Lindi na maeneo mengine. La kwanza kabisa, Serikali sasa inajenga miundombinu ya kusafirisha umeme, ule mkuwa kutoka Mtwara na kurekebisha miundombinu iliyoharibika hapa ambayo tumesema ya urefu wa kilometa 2016. Njia za miundombinu kutoka Mtwara hadi Newala, Tandahimba na maeneo mengine ilikuwa ni ndefu sana, kwa hiyo, hatua ya kwanza Serikali inaanza kujenga *transmission line* ya umbali wa kilometa 80 ambayo itakamilika mwezi Mei mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua ya pili inajenga kituo cha kupoza umeme kitakachokuwa Mnazi Mmoja maeneo

ya Lindi ambacho kitahudumia sana maeneo yote ya Newala, Tandahimba na maeneo mengine ili kupunguza tatizo la kukatika kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kwamba inarekebisha pia mashine ambazo zilikuwa mbovu kama nilivyoeleza na kununua nyingine mpya ili kufikia mahitaji halisi ambayo ni megawati 30 kwa wananchi wa Mtwara na Lindi na Wilaya zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na gharama za umeme. Gharama za umeme kwa manufaa ya wananchi wote ningependa niseme ifuatavyo; kwa vijijni kupitia mradi kabambe wa *REA* gharama za umeme za kuunganisha kwa wananchi ni shilingi 27,000/= tu basi hakuna gharama nyingine. Ningependa lieleweke hili ili kusudi wananchi wengine wasibambikiziwe bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo, zipo gharama za kutandaza nyaya kwenye nyumba. Hizo ni gharama zinaotegemea na ukubwa wa nyumba lakini pia zinategemea na mkandarasi waliokumbana nae. Tunachofanya kudhibiti hilo ni kuhakikisha sasa wakandarasi wote wanaounganisha nyaya kwenye numba za wateja sharti la kwanza lazima waidhinishwe na *TANESCO* na majina yao yabandikwe katika Ofisi za *TANESCO* ili ikitokea ulaghai tuweze kuwafuatilia. Hizo ni gharama za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upo mpango mwingine kwa wananchi wa kawaida ambao nyumba zao zina chumba kimoja hadi vinne. Tunawaptia chombo knachoitwa UMETA yaani maana yake Umeme Tayari Ukikiweka. Gharama yake ni shilingi 36,000. Kwa hiyo, nataka kuweka wazi kuhusu gharama kijijini. Lakini gharama halisi kwa maeneo ya mijini kwa umbali usiozidi nguzo moja ni shilingi 177,000/= na kwa mijini ni shilingi 320,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo muhimu ningependa kuyafafanua, lakini pia mambo mengine

inategemea sasa na mambo ambayo mteja pia anahitaji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi niulize nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inafanya kazi nzuri ya kuwapelekea umeme wananchi katika nchi yetu; na kwa kuwa kipindi kilichopita Serikali kwenye Jimbo la Makambako hususan vijiji vya Ikwete, Nyamande, Manga, Utengule, Mlowa, Mahongole, Kitandililo na Kifumbe iliahidi kutuletea umeme katika Awamu ya Pili na mkandarasi ambaye tulikuwa tumepewa alikuwa ni *LAC Export* na mkandarasi huyu baadae Serikali kupitia Bunge hili walisema wamemuondoa kwa sababu alikuwa hakidhi vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Serikali itatupeleka katika vijiji hivi nilivyovitamka umeme Awamu hii ya Tatu ili wananchi hawa waweze kupata umeme kama ambavyo wanapata sehemu zingine? Nakushukuru.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikubaliane na Mheshimiwa Sanga na nampongeza, kweli nilipomtembelea alinipa ushirikiano mkubwa na inaonesha Mheshimiwa Sanga pamoja na kwamba wananchi wanakuoenda, lakini na sisi tunakupenda kwa kazi unayowafanyia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli kabisa vijiji saba katika eneo la Makambako ikiwemo pamoja na vijiji alivyovitaja vya Ikwete pamoja na Kifumbe ilikuwa vipatiwe umeme kupitia mpango huo. Na kama utakumbuka Mheshimiwa Sanga, uko mradi unaojenga usafirishaji wa

umeme kutoka Makambako kupitia Madaba hadi Songea na ndiyo vijiji vilitakiwa vipatiwe umeme kutoka utaratibu ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata vijiji vyote vile, saba pamoja na vitongoji vyako vyote imeingia katika mpango wa *REA* ulioanza kutekelezwa katika maeneo ya Makambako pamoja na Njombe kuanzia tarehe 15 Januari, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwamabia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba utekelezaji wa Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu umeanza rasmi tangu tarehe 15 Januari, 2017 na tunachofanya sasa na wananchi na Wabunge ni kuzindua Mkoa hadi Mkoa ili kuwakabidhi wakandarasi Waheshimiwa Wabunge mliko ili na ninyi wote mkitusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Deo Sanga tumeshazinfua tangu tarehe 15 Januari na wananchi wako wa vijiji hivyo saba pamoja na kijiji cha Kifumbe wataanza kupata umeme kupitia mradi huu wa *REA* wa Awamu ya Tatu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la kukatika kwa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara halitofautiani na tatizo la kukatika kwa umeme katika Mkoa wa Kilimanjaro hasa Jimbo la Moshi Mjini. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuhakikisha kwamba wanatatua tatizo la ukatikaji wa umeme katika Jimbo la Moshi Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Arusha kulikuwa na tatizo la mara kwa mara la umeme. Lakini uko mradi mmoja unaoitwa *Trade Up*

unaotekeleza ukarabati wa miundombinu katika mikoa hiyo mitatu. Mheshimiwa Japhary nikuambie tarehe 22 Mei taratibu kabisa za kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Mji wa Kilimanjaro utakamilika kupitia mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa hatua ya pili tunajenga pia mradi wa kusafirisha umeme unaotoka Kinyerezi kwenda Tanga, unakwenda mpaka Namanga, lakini uko unaotoka hapa sasa kutoka SInginda kupita Manyara na kwenda mpaka Kilimanjaro wa kilovoti 400 ambao pia utaongeza nguvu ya umeme na kupunguza sasa kukatika katika kwa umeme kwa sababu ya *low voltage.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Japhary kuanzia mwezi Mei tunaweka kwamba kukatika umeme katika Mkoa wa Kilimanjaro utapungua kwa kiasi kikubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mkwajuni ambao ndiyo makao makuu ya Wilaya ya Songwe, kila wiki umeme upo siku tatu na umeme haupo siku nne mpaka hivi ninavyoongea, hata wiki iliyopita nilikuwa huko. Nini tatizo la kukatika katika kwa umeme hasa ule unaotoka Mbeya Lwanjilo, Chunya, Makongolosi mpaka Mkwajuni. Tatizo ni nini kila mwaka maana huu ni mwaka wa nne sasa hatuna umeme wa uhakika pale Mkwajuni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa maeneo mengi umeme tulionao haujitoshelezi ndiyo maana tunarekebisha na kuimaisha

miundombinu ikiwemo Mkoa wa Mbeya pamoja na mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua tuliyochukua kwa sasa tunajenga mradi wa kusafirisha umeme wa KV 400 kutoka Mbeya kupita Sumbawanga kwenda Kigoma hadi Nyakanazi, lakini huo huo utakwenda mpaka Bulyanhulu na Geita umbali wa kilometa 1,108.

Kwa hiyo, hatua hii itakapokamilika katika Mkoa wa Mbeya tatizo la umeme litapungua sana. Matarajio yetu, kufikia mwezi Julai, 2018 matayarisho, ujenzi pamoja na uimarishaji wa njia za kuimarisha umeme katika Mkoa wa Mbeya utakuwa umekamilika. Kwa hiyo, kuanzia Julai mwakani kukatika kwa umeme katika Mkoa wa Mbeya kutapungua au kutakoma kabisa kwasababu ya kutekelezwa kwa mradi huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mkwajuni siku hizi iko Songwe imegawanyika kwa hiyo naamini uliposema Mbeya ulikuwa unamaanisha Mbeya na Songwe kwa pamoja.

Mheshimiwa Mtolea, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa tatizo la kukatika katika kwa umeme lililopo Mtwara na Lindi linafanana kabisa na hali ilivyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke hasa katika Kata za Kurasini, Mtoni, Keko, Chang'ombe, Tandika Sandari, Buza na maeneo yote ya Yombo ambapo kila siku ni lazima umeme ukatike na pale inapokuwa na hali ya mawingu au mvua basi umeme hukatika kwa muda mrefu zaidi. Sasa wananchi wa Temeke wangependa kusikia majibu ya Serikali, ni lini tatizo hili litakoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika kujibu swali la nyongeza katika Mkoa wa Kilimanjaro, mtekelezaji anayerekebisha mitambo pamoja na miundombinu katika maeneo ya Temeke, Kurasini, Kigamboni pamoja na Kiwalani ni mradi mmoja. Lakini katika maeneo ya Temeke mwezi uliopita nilifatana na Mheshimiwa Mbunge wa Temeke, nimeenda kukagua mradi wa Temeke na Kurasini. Kinachofanyika sasa wanaimarisha na kuweka vikombe vipya kwa sababu maeneo ya Temeke, Kurasini yamezidiwa. Kwa hiyo, tunaongeza nguvu ya umeme ya kilovolti 220 kutoka 132, lakini kadhalika tunafupisha umbali wa nyaya uliokuwepo wa zaidi ya kilometa 57 ili ziwe chini ya kilometa 50 katika maeneo ya Temeke, Kurasini, Kigamboni pamoja na Kiwalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaratibu wa kukamilisha tarehe 27 Aprili, 2017 mradi utakamilika. Kwa hiyo, baada ya kukamilika kwa mradi huu maeneo ya Temeke, Kurasini, Kigamboni na maeneo ya jirani tatizo la umeme litapungua sana kwa kiasi kikubwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Jaku.

Na. 15

**Malipo ya *Corporate Tax* kwa Kampuni Zenye Matawi Zanzibar**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB (K.n.y. JAMAL KASSIM ALI)** Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mwaka 2013 zilikubaliana kuwa kodi ya *PAYE* kwa wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zote za SMT ambao wanafanyakazi Zanzibar kodi yao ya *PAYE* ikusanywe na *TRA* Zanzibar na kuiwasilisha kwa SMZ.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa kufanya hivyo kwa kampuni zote binafsi ambazo zina matawi/ofisi Zanzibar kulipia *Corporate Tax* ambayo kutokana na faida inayotokana na shughuli zao za biashara ndani ya Zanzibar ili kodi hiyo iende kusaidia masuala ya maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 66, kifungu cha 4 sehemu ya (a) na (b); Kodi ya Kampuni *(Corporation Tax)* ni kodi ya Muungano na inakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Kikatiba kodi zote za Muungano zinakusanywa na *TRA*. Hata hivyo, kampuni ambayo imesajiliwa Tanzania Bara na ikawa na matawi Zanzibar inatakiwa kulipa kodi ya kampuni *TRA* Bara. Iwapo kampuni imesajiliwa Zanzibar na ikawa na matawi Tanzania Bara inatakiwa kulipa Kodi ya Kampuni Zanzibar. Kwa msingi huo, Kodi ya Kampuni inatozwa sehemu ambapo kampuni imesajiliwa, yaani Tanzania Bara au Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutokuwa na afya naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri kuna ushahidi ambao kama utakuwa tayari kuja kuueleza kuwa kuna kodi zinalipwa Bara, je, utakuwa uko tayari kupokea ushahidi huo ili Zanzibar nayo inufaike kibiashara

kupata mapato hayo ili imalize deni lake la umeme inayodaiwa? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuna Tume ya Fedha iliyoundwa mwaka 2007 mpaka leo hiyo Tume ya fedha haijakutana kutatua matatizo hayo, je, ni lini kama Naibu Waziri utachukua hatua hizo ili kutatua tatizo hili la Tume ya Fedha ya Pamoja iliyoundwa nafikiria mwaka 2007 hadi leo karibu miaka 16 haijakutana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku maswali ya nyongeza yanatokana na swali la msingi, kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri majibu yale yanayotokana na swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kabisa kupata huo ushahidi anaosema na ikiwa tutajiridhisha ni kodi iliyotakiwa kukusanywa Zanzibar imekusanywa Bara tuko tayari kuirejesha Zanzibar, kwa hiyo, naomba tupate ushahidi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Fedha ya Pamoja najua imeundwa kama alivyosema na inafanya vikao vyake sasa pia nimeshangaa kusema kwamba tangu imeundwa haijawahi kufanya kazi. Nalichukua suala hili na kama Serikali tunalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Tunaipongeza Serikali kwa kukusanya kodi kwa kiwango ambacho ni cha juu sana, lakini wafanyabiashara wanatakiwa wajikisie makisio yao na ndio walipe kodi kutokana na vipengele ambavyo wameweka kwenye makisio.

Je, Serikali ina kauli gani juu ya malalamiko yaliyoko sasa hivi kwamba watumishi wa *TRA* wanakisia zaidi ya yale makisio ambayo wao ndio wanatarajia kufanya mauzo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani liko kwenye nguvu zako za kujibu japokuwa halitokani na swali la msingi, Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko hayo kuhusu watumishi wetu wa *TRA* na tumekuwa tukifanya vikao kuhusu suala hili. Naomba kuliharifu Bunge lako tukufu kwamba pia kumekuwa na tatizo la wafanyabiashara zetu kuleta taarifa ambazo sio sahihi ndio maana inapelekea kupata mvutano kati ya wafanyakazi wetu wa *TRA* na wafanyabiashara. Lakini kama Serikali tunasimamia uadilifu na kwa uhakika kabisa kinachotendeka ndani ya *TRA* ni kitu ambacho kinasimamiwa kwa maadili, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali King swali la nyongeza.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kodi hizo zinalipwa kwa kigezo cha usajili. Ukweli ni kwamba kampuni zote zinasajiliwa kutokana na *headquarter* alipo *regulators*. Kwa hiyo, mabenki mengi na makampuni ya simu yako Bara na *regulators* wake wako Bara, usajili wake unafanyika Bara wanalipia Zanzibar. Lakini ukweli upo kwamba mkaa na maiti haachi kulialia na mtegemea nundu haachi kununa, je, Serikali iko tayari kutumia kigezo cha *operations* za hizi kampuni kodi ikawa-*charged* kule ambapo zina-*operate?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Kijaji!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kodi ambayo tunaiita *corporate tax* inalipwa kule ambako kampuni imesajiliwa. Hilo alilolisema Mheshimiwa Ali King ni sahihi lakini pia naomba ndugu zangu tuweze kuangalia uhalisia ulivyo. Kwa mfano makampuni makubwa kama Kampuni ya Bakhresa, Kampuni ya *Zanzibar Insurance*, Kampuni ya Zantel zimesajiliwa Zanzibar na kodi ya mapato inalipwa kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hicho anachokisema naomba nimwambie Mheshimiwa Ally King kwamba hata hizi ambazo zinakusanywa kule Zanzibar, zinakusanywa huku Bara kwa pamoja zinaingia katika mfuko mkuu wa Serikali na kwa pamoja fedha hizi zinapoingia kwenye mfuko mkuu wa Serikali tunaweza pia kuhudumia Serikali zote za pande mbili ya Bara na Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fedha kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa sasa ni donda ndugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko ya Sheria ya *VAT* ya mwaka 2014 kama sikosei imepitishwa kwamba bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar hazitozwi ushuru hapa Tanzania Bara na wanatakiwa watoze ushuru kule Zanzibar ambako *ZRB* wanatoza ushuru wa asilimia 18. Lakini bado *TRA* Zanzibar wanawatoza wafanyabiashara hawa *trade levy* ya asilimia tano kusema kwamba bidhaa ile ile mfanyabishara wa Zanzibar anatakiwa ailipie asilimia 23 ya kodi, je, huku si kumuonea mfanyabiashara huyu wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Kijaji majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ameanza yeye mwenyewe kusema Sheria ya *VAT* tuliipitisha hapa na tunaitekeleza kisheria. Hilo analolisema la wafanyabiashara kwamba wanaonewa nimuombe Mheshimiwa Mbunge kama na yeye ana uthibitisho wa hilo analolisema aweze kutupatia ili tuweze kufanyia kazi. Lakini kitu ambacho kipo tunajua kodi zote zinatozwa kulingana na sheria zilizopitishwa na Bunge lako tukufu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji wa Wami - Chalinze**

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE** Aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu wananchi wa Halmashauri ya Chalinze wamekuwa katika sintofahamu juu ya lini mradi wa maji wa Wami - Chalinze utakamilika ili wananchi hao waweze kunywa maji safi kama walivyoahidiwa.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni lini mradi utakamilika?

(b) Kwa kuwa mradi huu umekuwa unakwenda taratibu sana; je, tatizo lake ni nini?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Benki ya Maendeleo ya Waarabu yaani *BADEA,* Washirika wa Maendeleo *(DPs)* kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* na Mkopo kutoka Serikali ya India kupitia *Exim Bank* kwa pamoja zimetoa jumla ya shilingi bilioni 164 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji Chalinze kwa Awamu ya I, II na III. Gharama ya utekelezaji wa miradi hiyo ni shilingi bilioni 23.4 kwa Awamu ya I, Awamu ya II ni shilingi bilioni 53.7 na shilingi bilioni 86.9 kwa awamu ya III.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa Awamu ya I na ya II ya mradi wa Chalinze jumla ya vijiji 88 vimenufaika

na kupelekea hali ya upatikanaji wa maji Chalinze kufikia asilimia 88 ya wakazi wote waishio katika eneo lote linalopitiwa na mtandao wa maji. Vijiji 12 vya Mwidu, Visakazi, Lulenge, Tukamisasa, Kinonko, Bwawani, Sinyaulime, Gwata, Ngerengere, Kidugalo, Kambi ya Kinonko na Sangasanga ambavyo vipo katika Awamu ya II vitaanza kunufaika na huduma ya maji ifikapo mwishoni mwa mwezi Aprili, 2017 baada ya kukamilika majaribio ya bomba kuu. Vijiji vitatu vya Kwang'andu, Kifuleta na Kwaruhombo vitaanza kupata maji baada ya mkandarasi kufanya maboresho ya pampu ambazo zimeonekana hazifanyi kazi ilivyotarajiwa. Mkandarasi ameagizwa kuhakikisha pampu hizo zinafanya kazi kabla Juni, 2017.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inatekeleza mradi katika Awamu ya III ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji, ujenzi wa mabomba makuu ya kusafirisha maji (kilometa 115), ujenzi wa mfumo wa mabomba yakusambaza maji (kilometa 1022), ujenzi wa matanki makubwa 19 na ujenzi wa vituo tisa vya kuchotea maji na ujenzi wa vioski vya kuchotea maji 351. Awamu hii kimkataba ilitakiwa iwe imekamilika tarehe 22 Februari, 2017, mpaka sasa ni asilimia 23 tu ya kazi ndiyo imefikiwa. Serikali imechukua hatua za kimkataba ikiwemo kutoa *notice* ya siku 100 ili aongeze kasi vinginevyo tutasitisha mkatabaifikapo tarehe 31 Mei, 2017.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete swali la nyongeza!

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ya mwanzo lakini pili nimpongeze pia na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuja kuyaona mambo yanayoendelea Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Chalinze wamechoka kusubiri maji na kwamba sasa imefikia sehemu sijui nisemeje maana yake Waziri yeyé mwenyewe ameyaona. Sasa je, Serikali pamoja na kutoa *notice* ya siku

100 imejipangaje kusimamia utekelezaji wa kusitisha mkataba huu, kwa sababu tunavyofahamu sisi kwa mahitaji ya matanki 19 ujenzi wa vituo tisa na vioski vya kuchotea maji 351 sina hakika sana kama huyu mjenzi anaweza akamaliza. Pamoja na hilo pia naomba nimkumbe Mheshimiwa Waziri kwamba mjenzi huyu ndiye yule ambaye amenyangwa *passport* na Mheshimiwa Rais kule Lindi, sasa je, Serikali imejipangaje juu ya *wayforward* baada ya kusitisha mkataba na mjenzi huyu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunapokea pongezi ambazo anazitoa kwa Waziri Mkuu kwa kuweza kutembelea mradi huu.

Kuhusu suala la *notice* tuliyoitoa kitu kinachofanyika sasa kwanza tulitoa barua kwa mfadhili ili kuomba *no objection* kwa sababu ni miradi ambayo ina ufadhili lazima wao waidhinishe kama unataka kusitisha mkataba na kwamba wao watakuwa tayari kuendelea kufadhili kazi zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tulichokifanya kwamba tumetoa *notice* ya siku 100 na tunafanya *monitoring* kufatilia kila siku kazi ambazo nazalisha, na sasa hivi na yeye mwenyewe anaweza kushuhudia ameongeza kasi ambayo wala hatukutarajia, kazi inakwenda kwa nguvu sana. Ikifika tarehe 31 Mei tutafanya tathmini kuangalia kwa *speed* hii anayofanya je, anaweza akamaliza katika muda mfupi, lakini kwa wakati huo huo Serikali imechukua hatua kwamba malipo yote ambayo yatakuwa yanatolewa anakatwa tozo ya ucheleweshwaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeweza kumwagiza Mhandisi Mshauri kwamba aandae makabrasha ya zabuni ikifika tarehe 31 Mei kama itakuwa kasi ile hairidhishi tunaajiri mkandarasi mwingine kwa sababu fedha zile za kufanya ile kazi zipo na hakuna fedha ambayo imelipwa kwa kazi

ambayo haijafanyika. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie wananchi wa Chalinze kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kukamilisha mradi huu wa maji Chalinze.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Masele swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Siku nne ama tano zilizopita mradi mkubwa wa kitaifa wa maji wa *KASHWASA* Shinyanga ambao una-*supply* maji Manispaa ya Shinyanga pamoja na mji wa Kahama ulikatiwa umeme na *TANESCO* kwa sababu ya kutolipa bili za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuuliza Waziri wa Maji nimekuwa nikishauri hapa kwamba Serikali itenge ruzuku ya kusaidia mradi huu ili kuwaondolea mateso wananchi wa Shinyanga, Kahama na Maswa, je, Waziri yuko tayari kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu kuhakikisha kwamba *KASHWASA* inasaidiwa ruzuku ya kuendesha mradi huo na kuwaondolea mzigo wananchi wa Shinyanga, Kahama na Maswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa utaratibu mamlaka za maji tumeziweka kwenye makundi daraja A, B, na C. *KASHWASA* ni daraja A, kwa maana kwamba inatakiwa iwe inalipa maji kutokana na mauzo ya maji. Sasa *TANESCO* wamekata deni ambalo walikuwa wanadaiwa na tatizo ni kwamba taasisi nyingi zilikuwa hazijaweza kulipa kwa wakati. Tunaendelea kusisitiza kwamba taasisi zote za umma lazima zilipe bili za maji ili kusudi kuwezesha mamlaka zetu zilipe *TANESCO*. Kwa hiyo, hilo lililotokea, limetokea lakini kwa hivi tunasema wasiyazalishe madeni mapya na tutafika mahali tutaanza kukatia hata hizo taasisi za umma ambazo hazilipi bili za maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini swali la nyongeza!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji inayosimamiwa kitaifa inasuasua katika maeneo mengi, katika Jimbo langu la Rombo kuna miradi miwili, Mradi wa Leto na Mradi wa Shimbi Mashariki ni ya muda mrefu sana na upatikanaji wa fedha umekuwa unasuasua. Katika kipindi hiki ambacho hali ya ukame imekuwa kubwa sana ukanda ambao hii miradi ipo una shida kubwa sana ya maji. Sasa je, Serikali iko tayari kupeleka fedha zote za hii miradi ili ipate kukamilika wananchi wa eneo lote la ukanda wa chini katika Jimbo la Rombo waweze kunufaika na miradi hii ambayo imechukua muda mrefu sasa kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Lwenge majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza anaelezea kwamba miradi kwenye eneo lake inasuasua, lakini tulishatoa maelekezo na nimetoa muongozo namna gani tutakwenda kutekeleza hii miradi hasa kwenye maeneo ya vijijini kwa maana ya utekelezaji wa Programu Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunakamilisha miradi inayoendelea na utaratibu ni kwamba wakandarasi wengi wamesharudi sasa, walikuwa wamesimama kwa sababu ya fedha zilikuwa hazipatikani kwa wakati, lakini sasa wamerudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na sasa hivi kila mkandarasi aliyerudi akileta *certificate* tumekuwa tunalipa kwa wakati kwa hiyo, tunataka tupate matokeo ya haraka miradi ikamilike kwa sababu hatuwezi kuleta fedha tu zikae kwenye Halmashauri ya Rombo wakati hakuna kazi inayofanyika. Tunapeleka mahali ambapo kazi inafanyika, ili tupate matokeo ya haraka wananchi wetu waweze kupata maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nikazie kusema kwamba, Mradi wa *KASHUWASA* wa Shinyanga sio mamlaka ni mradi na vilevile wananchi wa Mji wa Maswa leo sasa wanakwenda wiki ya tatu wanakosa maji kisa *TANESCO* imewakatia umeme kwa sababu hawajalipa bili ya umeme na wananchi wa Maswa wanalipa bili zao kwa muda unaostahili na maji wamekatiwa kwa sababu ya makosa sio ya kwao. Je, Mhesimiwa Waziri unawahakikishia ni lini wananchi wa Maswa na Shinyanga watapata maji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Masele, tunaposema Mamlaka za Maji, *KASHUWASA* ni Mamlaka ya maji katika daraja la kwanza ambalo kwamba, linatakiwa lisipate ruzusu ya kulipa bili ya maji kutoka Serikalini, anatakiwa alipe kutokana na makusanyo ya madeni, yaani ya watu wanaotumia maji yale. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu ambao tumepanga, tunazisaidia hizi mamlaka za daraja la C ambazo hazina wananchi hawawezi kuhumili gharama za uendeshaji wa miradi ile. Kwa hiyo, katika hii miradi midogo midogo, hii tunatoa ruzuku na kwenye bajeti tunatenga fedha na mwaka huu wa fedha tulitenga fedha, lakini na mwaka unaokuja tutatenga fedha kwa ajili ya kulipia ruzuku katika hizi mamlaka ndogo za daraja la C na B ambazo hazina uwezo wa kuweza kujiendesha. *(Makofi)*

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mamlama ya Maji ya Mji wa Karatu *(KARUWASA)* ina zaidi ya umri wa miaka mitatu, lakini uendeshaji wake umekuwa ukisuasua kwa sababu mamlaka hiyo bado haina bodi ya usimamizi; majina ya wajumbe waliopendekezwa kwenye bodi hiyo yalishapita kwenye ngazi ya Baraza la

Madiwani zaidi ya miezi sita. Ni lini bodi hiyo itaundwa ili isaidie uendeshaji wa mamlaka hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hizi mamlaka za bodi katika miji midogo zinaundwa chini ya TAMISEMI na ile miji ya mikoa na miradi ya kitaifa zinaundwa chini ya Wizara ya Maji. Sasa naomba nilichukue kwamba suala hili tuliangalie ni kwa nini mpaka leo bodi haijaundwa. Labda kutakuwa na tatizo, sasa siwezi kuwa na jibu sasahivi, nitakwenda kulifanyia kazi na nitamjulisha Mheshimiwa Mbunge ni wapi tumefikia kuhusu kuunda Bodi ile ya Maji katika Mji wa Karatu.

Na. 17

**Mradi wa Umwagiliaji - Mufindi Kaskazini**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** Aliuliza:-

Serikali imeweka pesa nyingi sana katika mradi wa umwagiliaji uliopo katika Kijiji cha Ikweha, Kata ya Ikweha, lakini unashindwa kuanza kwa kuwa Serikali imeshindwa kujenga bwawa.

(a) Je, ni lini mradi huu utakamilika ili kutoa ajira kwa vijana walio wengi katika Kijiji cha Ikweha?

(b) Je, Serikali itawachukulia hatua gani wakandarasi waliojenga mradi huu chini ya kiwango?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, leny sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza Skimu ya Umwagiaji ya Ikweha, Serikali ilitekeleza mradi huo kwa

awamu mbili. Awamu ya kwanza ilitekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 435.9 na awamu ya pili ilitekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 370.7. Baada ya kukamilika kwa awamu hizo kulikuwa na mapungufu mbalimbali ambayo yalibainika na yalitakiwa kurekebishwa ndani ya kipindi cha matazamio ya miezi 12 kilichotarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2016. Hata hivyo, kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa kazi alizokuwa amezifanya iliababisha ucheleweshaji wa marekebisho wa mapungufu hayo. Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na mkandarasi wamekubaliana marekebisho hayo yaanze kufanyika mwezi Aprili, 2017.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mkandarasi atashindwa kukamilisha marekebisho hayo yaliyo kwa muda wa matazamio wa miezi 12, Serikali itamchukulia hatua za kisheria kulingana na mkataba ili kumtoza tozo na kutolipa kazi ambazo ziko chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga mabwawa kama hatua muhimu ya kukabiliana na changmoto za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha usalama wa chakula kupitia kilimo cha umwagiliaji. Serikali katika Bajeti ya mwaka 2017/2018 itafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mabwawa mbalimbali ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji likiwemo hili la Ikweha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja na ombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Serikali, naomba kupata *commitment* ya Serikali, lini mradi huu utaanza kufanya kazi kwa sababu vijana wengi waliopo katika Kijiji cha Ikweha wanategemea sana kupata ajira katika eneo hili ukichukulia kwamba muda wa matarajio ya kukamilika kwa mradi huu uliishia mwezi Agosti, 2016 na sasa hivi Serikali imesema wataanza rasmi Aprili 17. Sasa ni lini mradi huu utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulikuwa unashughulikiwa kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi pamoja na wafadhili, Serikali Kuu ilikuwa bado haijajiingiza. Naomba nichukue fursa hii kumuomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa Bunge lako hili tukufu tuambatane nae aende akaone hali halisi na umuhimu wa mradi huu kwa ajili ya wananchi wa Kijiji cha Ikweha.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mgimwa kwa kufuatilia miradi hii ya umwagiliaji.

Pili, lini anasema utakamilika. Kama tulivyoeleza kwenye jibu la msingi, kwa sababu fedha hizi zilikuwa zimetolewa na wafadhili na ndio maana kulichelewesha kukamilisha marekebisho yanayotakiwa. Na kwa sababu wamekubaliana na Halmashauri waanze mwezi wa nne kwa hiyo, tunafikiria kulingana na kazi zenyewe ni ngapi zinazotakiwa kurekebishwa, siwezi kusema muda hasa, lakini natarajia kwamba, katika miezi 12 iliyokuwa imepangwa mwanzo ndio hiyo ina-*carry forward* kwamba tutaanza mwezi wa nne kurekebisha marekebisho ambayo yamefanyika ili kusudi mradi ule uweze kufanya kazi. Lakini pia mwaliko wa kutembelea mradi huo naupokea na tutakwenda kuutembelea na kuona hali halisi jinsi ilivyo.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tatizo la mradi wa umwagiliaji la Mufindi Kaskazini linafanana kabisa na tatizo la mradi wa umwagiliaji uliopo katika Halmashauri ya Songea katika Kata ya Subira na katika Mtaa wa Subira. Mradi huu ni wa muda mrefu, umeanza tangu mwaka 2008 na mpaka sasa hivi bado haujakamilika, pesa zilizotumika mpaka sasa hivi ni shilingi milioni 585 na bado panatakiwa zaidi ya shilingi bilioni moja ili kukamilisha mradi huu. Je, Serikali imetenga kiasi gani kwa ajili ya kukamilisha mradi huu kwa kipindi hiki cha Bajeti ya mwaka 2017/2018? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli miradi mingi ya umwagiliaji ina matatizo. Na ina matatizo kwa sababu, kwanza kulikuwa na udhaifu katika usimamiaji katika sekta hii, hii miradi ya kilimo. Na miradi mingi ilikuwa ina ufadhili wa *JICA.* Kwa hiyo, kulikuwa na *weakness* katika usimamizi, yaani ulikuwa dhaifu na ndio maana utekelezaji wake haukwenda kwenye viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nikiri tu kwamba katika bajeti ya mwaka huu wa fedha tulitenga fedha kwa ajili ya kufanyia mapitio ya miradi yote ya umwagiliaji, ili kwanza tuweze kuirekebisha iweze kufanya kazi iliyokusudiwa, hiyo ndio kazi ambayo inaendelea sasa hivi. Lakini pili, tulikuwa tunafanya usanifu wa miradi mipya ya umwagiliaji, sasa kwa sasahivi siwezi kukwambia bajeti ya mwaka 2017 ni kiasi gani, lakini nitakapowasilisha bajeti yangu najua utaunga mkono ili kusudi tuweze kukamilisha huu mradi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malapo nilikuona.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa vile Waziri amekiri kwamba, miradi mingi ya umwagiliaji ilikuwa na matatizo sasa je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu wakandarasi na wote waliohusika kufanya ubadhirifu wa pesa hizo nyingi, hasa ukizingatia kuna mradi wa umwagiliaji kule Kitele, Jimbo la Mtwara Vijijini mkoani Mtwara, ambalo kwa kweli wananchi walijitolea eneo lao, lakini mradi umejengwa chini ya kiwango, mifereji ina nyufa na ule mradi haujaanza kutumika. Nini kauli ya Serikli kuhusu miradi hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hii miradi tunaifanyia mapitio, lakini pale itakapoonekana mkandarasi au kuna mtu yeyote amefanya ubadhirifu, Serikali itachukua hatua zinazostahiki kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, naomba asiwe na wasiwasi, lakini lengo kubwa hasa la Serikali ni kuhakikisha kwamba miradi hii tunaikamilisha ifanye kazi iliyokusudiwa kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ngara yapo mabonde matano ambayo Serikali iliyaainisha kwa ajili ya kuanzisha skimu ya umwagiliaji. Upo mradi katika Bonde la Vigombo ambao mradi huo ulianza kutekelezwa na ulitakiwa ukamilike mwaka 2014, lakini mpaka sasa haujakamilika. Haitoshi, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilitenga takribani shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kutekeleza miradi katika mabonde mawili, Bonde la Mngozi, Kata ya Nyakisasa na Bonde la Muhongo katika Kata ya Bukiliro, lakini mpaka dakika hii tuko *quarter* ya nne hakuna hata senti moja ambayo ilishapelekwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli ya Mheshimiwa Waziri kwa wananchi wa Jimbo la Ngara kuhusu upelekaji wa fedha na ili kuweza kutekeleza miradi hii kama ilivyopangwa katika bajeti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kuna miradi ambayo inaendelea kwenye mabonde hayo anayoyaelezea. Lakini kwa sababu wanataka kujua lini ni vizuri hata mimi nikapata nafasi ya kuingia kuuangalia mradi maana siwezi kujua miradi

yote lini itakamilika. Lakini lengo la Serikali ni kwamba, miradi yote tutaikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, na suala la kupeleka fedha; fedha hatuzipeleki tunalipa *certificate.* Tumeshafanya mambo ya kupeleka fedha halafu unakuta fedha zinakaa hazishughuliki vyovyote. Tunataka matokeo kwa hiyo, fedha tutapeleka kulingana na utekelezaji wa mradi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa dhamira ya Serikali ni kujenga Taifa la Viwanda na sekta ya kilimo kuwa ni muhimu. Katika Halmashauri ya Mji wa Nzega tumekuwa na mradi uliokuwa unasimamiwa na Shirika lililokuwa linaitwa *NZEDECO* miaka ya 1970 na miaka ya 1980 la umwagiliaji katika Kata ya Idudumo, mradi huu sasa hivi umekufa. Vilevile katika Halmashauri ya Mamlaka Ndogo ya Mji wa Igunga nako katika Bwawa la Imamapuli limejaa tope.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba miradi hii miwili katika Halmashauri hizi mbili katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 wanatenga fedha kwa ajili ya kuifufua miradi hii ili wananchi wa maeneo hayo waweze kufaidika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ipo miradi mingi ambayo inaendelea nchi nzima na ni kwamba ni suala la Wizara yenyewe kuweka vipaumbele kwa sababu katika miradi huwezi ukatekeleza yote kwa wakati mmoja kutokana na upatikanaji wa fedha. Na kama anasema kwamba je, tuko tayari kutenga fedha kwa mwaka huu wa fedha unaokuja; itategemeana na mawasilisho ya Wilaya ya Nzega, kwa sababu ninyi ndio

mnaleta mapendekezo na vipaumbele katika Wilaya yenu. Kwa hiyo, kama mkiweka hii ndio kipaumbele Serikali basi itaangalia namna ya kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

Na. 18

**Uhamishaji wa Mipaka ya Msitu – *TFS* - Geita**

**MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU** Aliuliza:-

Wakala wa Misitu Tanzania amehamisha vigingi vya mipaka ya misitu vilivyowekwa tangu mwaka 1974 na kuviweka katikati ya vijiji kwa kufuata ramani ya mwaka 1984, vijiji ambavyo vina *GN* ya Serikali na vinatambuliwa na hata Mheshimiwa Rais amezuia zoezi hilo, lakini hakuna kilichofanyika hivyo kuwafanya wananchi wa vijiji hivyo kuishi maisha ya mashaka na sintofahamu.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Msitu wa Hifadhi wa Geita wenye ukubwa wa hekta 47,700 ulisajiliwa kwa ramani namba Jb 146 ya mwaka 1952 na ulitangazwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Namba 110. Sehemu kubwa ya msitu huu ipo kwenye miteremko ya milima ya Geita inayozunguka mji wa Geita sehemu ya Magharibi, Kaskazini na Kaskazini Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1984 Serikali ilifanya mapitio ya soroveya ya mipaka ya msitu kwa lengo la kuweka alama kwa kutumia ramani iliyoanzisha msitu huo. Katika mapitio hayo ilibainika kuwa mpaka halisi wa msitu kwa mujibu wa sheria umepita katikati ya vijiji vilivyoanzishwa na

kusajiliwa mwaka 1974 wakati wa *operation vijiji.* Alama za mipaka zikawekwa kufuata mpaka huu halisi na hivyo kusababisha eneo ambalo wananchi walikuwa wameanza kuishi na kufanya shughuli za kibinadamu na baadaye kusajiliwa kuwa vijiji kuangukia ndani ya eneo la msitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kubaini tatizo hilo Serikali haijafanya *operation* yoyote ya kuwaondoa wananchi katika maeneo hayo, bali ipo katika mjadala unaotafuta njia za kutatua tatizo hili bila ya kuleta athari hasi na kubwa kwa maisha ya wananchi. Aidha, Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuwa na subira wakati Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita inaendelea kutafuta suluhisho la mkanganyiko uliojitokeza kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma Kasheku, swali la nyongeza.

**MHE. MUSUKUMA J. KASHEKU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilitaka tu kumwambia kwamba, yale aliyoyajibu hapa si sawa na uhalisia ulioko kule Jimboni. Wananchi wangu wa vijiji vya Bugurula, Kasota, Nyawirimila, Sungusila na Kakubiro, wamewekewa matangazo mwezi mmoja uliopita na wakapelekewa barua za kuondoka kwenye vijiji ambavyo tayari vina shule na sasa Waziri anasema wao hawakuwa na huo mpango na hawajafanya wanaendelea na utaratibu na wameweka vigingi. Nilikuwa nataka kujua Waziri kama hizi taarifa alizozitoa ni sahihi ili niwaambie wale wananchi wangu kule wayang'oe yale matangazo yaliyowekwa kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na mkanganyiko wa mipaka ya vijiji na mapori ya hifadhi kumesababisha mpaka tunavyozungumza sasa kuna operesheni zinafanyika kwenye Mkoa wa Geita na Mkoa wa Biharamulo, Serikali ilitoa tangazo la siku tatu wananchi waondoe mifugo iliyopo kwenye hifadhi; siku tatu ng'ombe zitoke kwenye eneo la hifadhi kana kwamba hizi ng'ombe

sijui zina mota miguuni, lakini wananchi wa Kisukuma hawakuwa na tatizo walitii amri bila shuruti.

Na kwa kuwa waliopo kule wahifadhi wameidanganya Serikali kwa kuwaambia kuna mifugo milioni 60 na kule hakuna mifugo milioni 60; wamezikosa baada ya kupewa hiyo bajeti ya operesheni wakaikosa mifugo wananza kukamata sasa kilometa saba kwenye vijiji na wakati kuna *beacon* zinazoonesha mipaka ya kijiji. Je, Waziri husika anatoa kauli gani kwa wananchi ambao wamekamatiwa ng'ombe zao Ngara, Katente na Chato walioko mahakamani na wameshapewa hukumu ya ng'ombe zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na kwa hiyo kwa kiasi kikubwa anafahamu uzito, upana na ukubwa wa changamoto inayohusiana na suala la uhifadhi na muingiliano wa shughuli za kibinadamu katika maeneo mbalimbali nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii ni kubwa na haifanani kutoka mahali pamoja hata mahali pengine. Yapo matatizo yanayohusiana na wakulima na yapo matatizo yanayohusiana na wafugaji.

Katika swali lake la msingi Mheshimiwa Mbunge alizungumzia juu ya suala la maeneo ya vijiji ambayo yamo ndani ya hifadhi ya Geita na kweli lilikuwa ni suala la mipaka baina ya vijiji na maeneo hayo husika. Na kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi ni kwamba Wizara yangu kwa niaba ya Serikali haijafanya operesheni yoyote ya kuondoa wanavijiji katika maeneo hayo. Lakini nimesikia alivyosema kwamba kuna matangazo yamebandikwa huko ambayo sisi kama Wizara hata ninaposimama wakati huu mahali hapa bado hatuwezi kuthibitisha uwepo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hapa kwa kuwa Serikali ni pana iko mamlaka ya Wilaya, Mkoa na ipo Serikali Kuu kupitia Wizara, sote sisi ni Serikali. Baada ya hapa nikutane naye ili tuweze kufuatilia matangazo hayo juu ya uwepo wake na uhalali wake ili tuweze kujua namna ya kuweza kushughulikia tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu swali lake la wale wafugaji na mifugo katika maeneo ya Geita, Biharamulo na maeneo mengine ambapo zipo operesheni zinaendelea sasa hivi zikiendeshwa na mamlaka za Mikoa na Wilaya huko zilipo, kama nilivyotoa maelezo katika jibu langu la msingi, migogoro ipo katika maeneo mengi, lakini kila mahali, kila mgogoro ni wa aina yake; chanzo tofauti, ukubwa tofauti na kwa hiyo tarajia kwamba utatuzi wake pia utakuwa upo tofauti. Katika maeneo aliyoyataja uingiaji wa mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa ni mkubwa sana tena uliopelekea hata kuingia kwa mifugo kutoka nchi jirani na yeye amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali kupitia Mamlaka ya Mkoa imeendelea kufanya operesheni hizo kwa sababu kimsingi hatua za Serikali tulizotangaza kwamba zinaendelea kuchukuliwa haziwezi kukamilika leo au kesho kwa sababu zinafuata taratibu za kushughulikia changamoto za Kiserikali ambazo aghalabu huchukua muda mrefu. Katika kipindi hicho tukiacha ng’ombe waendelee kubaki katika maeneo hayo ya hifadhi, wakati utakapofika tumekwishapata ufumbuzi wa nini kifanyike hifadhi hizo hazitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge utaratibu ambao unaendelea hivi sasa wa Serikali wa kushughulikia changamoto hizo kwa uzito wake na katika maeneo ambayo athari ni kubwa huo utakuwa ni utaratibu wa Serikali na aendelee kuunga mkono jitihada za Serikali za kuamua kusimamia uhifadhi kwa maslahi ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kutakuwa na jambo lingine ambalo ni mahususi kuhusiana na hatua hizo ambazo Serikali inachukua katika ngazi hizo za Mikoa na Wilaya basi anaweza kulileta, nimesema yeye ni Mjumbe wa Kamati inayosimamia maliasili kwahiyo tunaweza kupokea maoni yake juu ya namna bora zaidi ya kuweza kushughulikia tatizo hili lakini kwa mujibu wa sheria. Katika hili sheria, kanuni na taratibu zitazingatiwa katika kushughulikia changamoto hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche naomba ukae, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nitoe majibu ya ziada pamoja na majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msitu katika Wilaya na eneo lilozunguka Mji wa Geita limefikishwa pia kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Geita na maazimio yaliyofikishwa yameletwa kwetu kwa ajili ya kufikiria ni namna gani katika maeneo ambayo watu wanaishi tunaweza kupunguza eneo la msitu kwa ajili ya matumizi mengine ili kukidhi hali halisi ya Mji Mkuu wa Mkoa ambao sasa uko pale Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili tunaendelea kulizungumza na Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali ya Mkoa na Wilaya inapoongea na Wizara kuhusu msitu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili; wapo ng'ombe ambao ni wengi sana katika maeneo ya misitu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Mifugo hii ipo

kwenye maeneo ya hifadhi kinyume cha sheria zetu; kinyume cha Sheria ya Uhifadhi wa Misitu Na. 5 ya mwaka 2009 kifungu cha 21(1). Na wananchi hawa wanajua kwamba wapo kwenye Hifadhi za Taifa kinyume cha sheria; walipewa muda wa kuondoka na tangazo la Mkoa na muda ule ukamalizika. Huwezi kusema mtu ambaye anafanya makosa ya kisheria kwamba hakupewa muda wa kutosha wa kufanya makosa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii kuwashauri wafugaji wote ambao wana mifugo yao ndani ya maeneo ya Hifadhi za Taifa kinyume cha sheria zetu kwamba watoe mifugo hiyo mapema iwezekanavyo kabla Serikali haijachukua hatua ya kisheria kudhibiti mifugo hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa mara nyingine kwa kuniona na kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza kwa niaba ya watu wa Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GN* hizi zilizotangaza haya maeneo na kuweka mipaka ya mapori ni ya miaka 1984; vijiji vingi ni vya miaka ya 1970, 1975 na kuendelea. Kwa hiyo, *GN* hizi zimetangazwa vijiji vikiwepo ukichukua Kata kwa mfano ya Kwihancha, Goronga na Nyanungu vimepakana na Pori la Serengeti; vijiji vyote vya maeneo haya ni vya miaka ya 1970 na vimesajiliwa vina usajili. Lakini watu wa Serikali wameanza kuhamisha kwa kutumia *GN* miaka ya 1990 mpaka sasa hivi wanazidi kurudisha watu nyuma, watu hawana maeneo ya kulima wala ya kuchungia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waziri watatue hili tatizo kwa haraka ili watu waendelee kuishi maisha yao ya kawaida na wasiendelee kuona wafugaji kwamba ni wahaini katika nchi yao, wawaruhusu ng'ombe wao waendelee kuchunga kwenye maeneo ambayo ni ya vijiji vyao kihalali na kisheria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani hilo lilikuwa ni wazo sina uhakika kama unataka kulitolea majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema kwa kiwango kikubwa yale yalikuwa ni maoni au ushauri lakini ni vyema sauti ya Serikali ikasikika na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kufanya marekebisho madogo tu kwamba sio vyema kujumuisha au kutoa kauli ya jumla kwamba *GN* zote ni za miaka 1980. Nadhani katika eneo mahususi analolitaja inawezekana ipo hivyo lakini utaratibu ambao utaweza kutufikisha mahali ambapo patakuwa ndio pana usahihi zaidi ni kwa kuchambua kila kesi kwa kesi na kila hoja kwa hoja kwamba eneo fulani linahusishwa na *GN* namba fulani, tutakwenda kuiangalia kwamba ni ya mwaka gani ili tuweze kujua eneo lililohifadhiwa na kijiji kilichopo kipi kilitangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo kutangulia au kuja baadae pengine inaweza kuwa sio hoja ya msingi sana; hoja ya msingi itakuwa ni uhifadhi kwa maslahi ya Taifa. Na hivyo ndio maana tumesema kwamba tunayo tume ambayo inaendelea kufanya kazi ambayo itahusisha pia na kufanya mapitio ya hayo yote tunayoyazungumzia. Kamati ambayo nimesema jana wakati najibu swali, lakini narudia tena leo ipo katika hatua ya kupitiwa na Makatibu Wakuu na baada ya pale itakwenda kwenye hatua ya Mawaziri halafu baadae kwenye ngazi za mamlaka za juu za Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa tatizo lililopo katika misitu ya Geita linafanana sana na tatizo lililopo katika Msitu wa Shume ambapo katika vijiji vya Shume, Nywelo na Mkuhnyi ambavyo vipo katika Kata ya Manolo navyo eneo la Msitu wa Hifadhi wa Shume umeingia katika maeneo ya vijiji ambako

wananchi mara nyingi ndiko wanakofanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tatizo la mgogoro huu pia limeripotiwa katika Randama ya Wizara ya Ardhi. Je, ni lini sasa Serikali itakaa na wananchi hawa wa vijiji vya Shume, Nywelo pamoja na Mkunki ili angalau waweze kutatua tatizo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia, tumepokea shamba la msitu wa kupandwa wa Shume uliopo katika maeneo yale ya vijiji alivyovitaja vya Shume, Nywelo na Mkunki. Ni suala ambalo kama alivyosema mwenyewe limeorodheshwa kwenye orodha ya maeneo ambayo yanatakiwa kushughulikiwa chini ya orodha ya migogoro ya ardhi iliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana kwa kutukumbusha licha ya kwamba lipo kwenye orodha na kwa kweli kwa namna ambavyo anaweza kuwasemea wananchi ya maeneo haya kama mwakilishi wao na nimuahidi sambamba na kazi inayoenda kufanyika chini ya kamati iliyoundwa; mimi na yeye tutapanga tutaweza kwenda kwenye hili eneo tukaangalie uhalisia ili tuweze hata kuishauri hiyo kamati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kuna tatizo pia la mipaka kati ya *TFS* na vijiji Wilayani Kondoa; vijiji vya Mnenia, Masanga, Itolowe na Kasese ambapo *beacon* za *TFS* zimeingilia katika mashamba ya wanavijiji hawa. Sasa ningependa kujua Serikali ina mkakati gani au ni lini itarekebisha tatizo hili ambalo linawaacha wanavijiji hawa njia panda? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia akisema kwamba katika vijiji alivyovitaja *beacons* za *TFS* kwa kauli yake zimeingia katika mashamba ya wananchi kwenye vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kwamba hii ndio sababu tumeunda kamati maalum kwa sababu kusema tu moja kwa moja kwamba *beacons* zimeingia kwenye maeneo ya mashamba ya watu bila kuangalia kwamba upo uwezekano mashamba ya watu yameingia ndani ya maeneo ya hifadhi haitakuwa sahihi katika hatua hii. Kwa hiyo, tuipe nafasi Serikali iweze kuendelea kufanya kazi ya kwenda kufanya utafiti wa kwenye *site* wa kuangalia uhalisia ulivyo tukipima kwamba ni kipi kimeingia upande upi lakini wakati huo huo tukiangalia zaidi maslahi ya hifadhi ambayo ndio *priority* kwa Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malocha swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana; lipo tatizo kubwa kati ya *Uwanda Game Reserve* na vijiji vya Kilangawana, Maleza, Legeza, Mpande, Ilambo, Mkusi, Iweliamvula na Ngomeni. Kwa watu wa *TFS* kuhamisha mipaka inayotambulika toka enzi za nyuma na kusogeza katikati ya vijiji. Tatizo hili ni kubwa sana na mimi nilishaenda mara kadhaa kumwambia Waziri kwamba naomba afike asikilize pande zote mbili kwa sababu ninachokiona hawa askari wa *TFS* ni kama wanagandamiza wananchi wakati jambo lipo wazi. Je, ni lini Serikali itatuma uongozi wa kwenda kuangalia haki juu ya wananchi wale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, anazungumzia juu ya suala la *Uwanda Game*

*Reserve* na ujirani wake na vijiji vilivyopo jirani na eneo hili la hifadhi. Na hoja yake inafanana na zile hoja zilizotangulia pale mbele kwamba mipaka iliyowekwa na *TFS* katika miaka ya karibuni au katika siku za karibuni imeingia ndani ya maeneo ya vijiji.

Kama nilivyosema hapo awali kwamba sio vema kwenda moja kwa moja na kutoa kauli ambayo inaonekana kama ni ya uthibitisho au ni ya ukweli kwamba mipaka ya hifadhi ndiyo iliyoingia kwenye maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niweze kusema jambo moja tu hapa kwamba tuelewane kitu kimoja kwamba mipaka tunayoizungumzia ya miaka mingi haikuwa na alama; kwa hiyo, kuna suala la kuweka mpaka kuwepo lakini kuna suala pia la mpaka kuwekewa alama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya karibuni kilichofanyika au kinachoendelea kufanyika ni kuweka alama za kudumu hizo *beacons* au maboya au unaweza kutafuta lugha nyingine yoyote ya Kiswahili, lakini ni alama zinazoonekana. Sasa wakati wa kuweka alama zinazoonekana Serikali inafuata mipaka ambayo ipo kwa mujibu wa maandishi kwa kutumia *GPS coordinates* kwenye ramani ambayo haikuwa imewekewa alama. Sasa kwa kuwa wananchi hawakuiona ile mipaka kwa alama zinazoonekana licha ya kwamba kwa mujibu wa sheria zipo kwenye ramani, sasa hivi wananchi wanadhani kwamba alama hizo zimehama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba alama hizo zinawekwa mahali pale ambapo ndipo kwa mujibu wa sheria alama hizo ndipo zilipo na kwa hiyo sasa ni vema tukasubiri utaratibu unaofanyika na Serikali wa kwenda kuweka alama kwenye maeneo hayo kwa sabau kuweka alama sio maana yake tayari hatua za mwisho zimeshafanyika za kuweza kuwahamisha wananchi; tunaweka kwanza alama kutambua maeneo hayo halafu baada ya pale tunaweza kuendelea na kuelimishana kwamba kwa nini mpaka upo hapa na sio pale.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Nichukue fursa hii kwanza kuwaomba radhi Wabunge ni wengi sana wenye shida hasa kwenye mambo ya maji, lakini sasa nafasi hazitoshi kila Mbunge kupata nafasi ya kuweza kuelezea tatizo lake. Lakini naamini kwa sababu Bunge hili ni la Bajeti kila Mbunge atapata nafasi ya kuangalia kwenye bajeti Jimbo lake limeangaliwa kwa namna ipi. *(Makofi)*

Lakini linalofuata ni matangazo; tangazo la kwanza ni la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi ambao wamekuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wa Waheshimiwa Wabunge, lakini pia wanafunzi mliokuja kujifunza.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yanayofuata ni matangazo ya kazi. Wajumbe wa Kamati Kuu ya Utendaji Chama wa Wabunge Wanaopambana na Rushwa *(APNAC)* Tanzania leo tarehe 5 Aprili, 2017 saa saba mchana katika ukumbi namba 227 uliopo katika Jengo la Utawala Ghorofa ya Pili, kutakuwa na Kikao cha Kamati Kuu. Kwa hiyo, mnaombwa na Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania Mheshimiwa George Huruma Mkuchika kwamba mhudhurie kikao hicho wajumbe wa mkutano huo.

Tangazo lingine ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuwa leo tarehe 5 Aprili, 2017 saa saba mchana katika Ukumbi wa *Utawala Annex* yaani *dispensary* kutakuwa na kikao cha Kamati hii. Kwa hiyo, Makamu Mwenyekiti, anawatangazia na anaomba mhudhurie.

Tangazo lingine linawahusu Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, Katibu wa Wabunge cha Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jasson Rweikiza anawatangazia Wabunge wa CCM, kuwa kutakuwa na kikao cha *caucus* saa 5.30 leo Jumatano tarehe 5 Aprili, 2017 katika Ukumbi wa

*NEC* Jengo la *White House* na mnaombwa wote kuhudhuria bila kukosa.

Tangazo lingine Mheshimiwa Daimu Mpakate, amepoteza *remote* ya gari yake jana, anaomba aliyeiokota tafadhali amjulishe na jana tulikaa hapa muda mrefu sana. Kwa hiyo, kuna uwezekano katika yale masaa tisa Wabunge walitembea tembea mwingine pengine aliondoka nayo amtazamie tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 6 Aprili, 2017 saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.04 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 6 Aprili, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*